# NDOA ZA UTOTONI TANZANIA



*Wape nafasi wachanue*

Msichana Initiative
Unleash Your Potential

Twaweza
ni sisi



# Tafakari

Je, tunashughulikia vipi sababu za kiuchumi zinazochochea ndoa za utotoni?

Je, kuna uhusiano wowote kati ya ukatili wa kingono kwa watoto na ndoa za utotoni?

Je ndoa za utotoni wakati mwingine zinaweza kuwa ni matokeo ya watoto kushambuliwa na kufanyiwa ukatili wa kingono na mambo haya kutatuliwa kifamilia au kijamii kupitia kuwafungisha ndoa?

Je, ni kwanini nchi jirani zimeweza kupunguza tatizo la ndoa za utotoni kwa haraka zaidi kuliko ilivyo kwa Tanzania?

Je, ni mahusiano gani ya kimamlaka kwa watu wazima yanayochochea ndoa za utotoni?

Je, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa ili kusaidia wanawake ambao wameolewa wakiwa bado watoto?

Ni kwanini jinsi moja ndio huathiriwa vibaya zaidi na ndoa za utotoni?

Endapo sheria itabadilishwa ili ndoa za utotoni ziwe hazikubaliki kisheria Tanzania, hatua hii itamaliza tatizo la ndoa za utotoni?

Unapaswa kufanya nini ukisikia kuhusu ndoa ya utotoni katika familia au jamii yako?

# Ndoa za Utotoni Tanzania

## Utangulizi

Kitini hiki cha mambo muhimu kinachunguza suala la ndoa za utotoni nchini Tanzania, ndoa zinazotafsiriwa kama ni hali ya kuishi katika muunganiko rasmi wa ndoa au usio rasmi kabla ya kutimiza umri wa miaka 18. Kinaangalia sababu zinazochangia kuendelea kuwepo kwa ndoa za utotoni, na pia baadhi ya madhara ya ndoa za utotoni kwa wahusika na taifa kwa ujumla.


Takwimu hizi zinatokana na vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoka kwenye taarifa ya utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia na kuchapishwa kwenye chapisho la Tanzania Economic Update la mwezi Januari 2019. Takwimu nyingine zimetoka kwenye taarifa ya utafiti wa Idadi ya watu na huduma za Afya ujulikanao kama Demographic and Health Survey (DHS) uliofanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa mwaka 2015-16, na takwimu nyingine kutoka utafiti wa Twaweza wa Sauti za Wananchi unaofanyika kupitia simu za mkononi kuhusu uzoefu na maoni ya wananchi. Pia unajumuisha nyaraka mbalimbali kutoka kwenye maazimio muhimu ya Kimataifa na Kikanda ambayo Tanzania imeridhia na kutia saini, pamoja na maelezo ya kesi ya kisheria juu ya ndoa za utotoni nchini Tanzania.

## Mambo 16 muhimu


**Jambo la 1. Tanzania imepiga hatua katika kupunguza ndoa za utotoni, ingawa nchi jirani zimefanikiwa kupiga hatua kwa haraka zaidi**

Wanawake watatu kati ya kumi wenye umri wa miaka 18-22 (32%) nchini Tanzania waliolewa kabla ya kutimiza miaka 18, idadi hii ni pungufu kutoka kwenye idadi ya wanawake wanne kati ya kumi (41%) wenye umri wa miaka 41-49.

Hata hivyo, nchi jirani zimepata mafanikio kwa haraka katika kupunguza tatizo la ndoa za utotoni, baadhi ya nchi hizi ni pamoja na Uganda, Zambia, Kenya na Rwanda.



**Asilimia ya wanawake walioolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18**





**Chanzo:** mkusanyo wa taarifa za Kiuchumi za Benki ya Dunia (World Bank Tanzania Economic Update) Januari 2019, kwa kutumia data za DHS za mwaka 2015-2016


**Jambo la 2. Mwanamke mmoja kati ya watatu ameolewa akiwa na umri wa miaka 18, mmoja kati ya ishirini akiwa na umri wa miaka 15**

Mwanamke mmoja kati ya watatu (31%) mwenye umri wa miaka 20-25 nchini Tanzania aliolewa akiwa na umri wa miaka 18, idadi hii imepungua kutoka wanawake wanne kati ya kumi (39-41%) miaka ishirini iliyopita. Hata hivyo, idadi ya wanawake ambao huolewa wakiwa na umri wa miaka 15 imebaki kuwa kubwa, kwa karibu mwanamke mmoja kati ya wanawake ishirini (5-6%). Umri wa wastani wa kuolewa umeongezeka kidogo, kutoka miaka 18.7 hadi 19.7.


**Asilimia ya wanawake wenye miaka 20-24 walioolewa wakiwa na umri...**




**Wastani wa umri ndoa ya kwanza, kwa wanawake wenye miaka 20-24**





**Chanzo:** DHS 1999, 2004-05, 2010, 2015-16



**Jambo la 3. Ndoa za utotoni zinafanyika zaidi maeneo ya vijijini, katika jamii masikini, na katika mikoa ya magharibi, kusini na kaskazini-magharibi mwa Tanzania**

Wanawake wanne kati ya kumi (37%) wenye umri wa miaka 15-49 wanaoishi Tanzania vijijini waliolewa wakiwa watoto, ikilinganishwa na wanawake wawili kati ya kumi (21%) wanaoishi maeneo ya mijini. Ndoa za utotoni pia ni suala la kawaida zaidi katika mikoa ya magharibi mwa nchi kwa (42%), ukanda wa kusini (42%) na kanda ya ziwa (39%). Wanawake wanaoishi katika kaya masikini (46%) wana uwezekano mkubwa mara tatu zaidi wa kuolewa kwa mara ya kwanza wakiwa bado watoto kuliko wanaoishi katika kaya tajiri (16%).


**Asilimia ya wanawake miaka 15-49 walioolewa wakiwa watoto, kwa maeneo walipo na utajiri:**




**Chanzo:** DHS 2015-16, , takwimu zimechambuliwa na mwandishi


**Jambo la 4. Kwa wasichana walioolewa wenye umri wa miaka 15-19, karibu wote hakuna anayeendelea na masomo shuleni kwasasa**

Karibu wasichana wote (99%) walioolewa katika umri wa miaka 15-19 nchini Tanzania hawaendelei na masomo shuleni, ni 1% tu ndio wanaendelea na



shule. Kwa wanawake wa rika lilelile ambao hawajaolewa, karibu nusu yao (45%) wanaendelea na masomo shuleni.

**Wasichana umri miaka 15-19 kwa hali ya kusoma na Kuolewa**





**Chanzo:** World Bank Tanzania Economic Update Jan 2019, kwa kutumia takwimu za DHS za mwaka 2015-2016

**Jambo la 5. Kuna uhusiano mkubwa kati ya umri wa kuolewa na mafanikio ya kielimu**

Mwanamke mmoja kati ya ishirini mwenye umri wa kati ya miaka 15-49 aliyeolewa akiwa mtoto amepata elimu ya sekondari, ikilinganishwa na robo (28%) ya wanawake ambao wameolewa wakiwa na umri wa miaka 20 au zaidi na nusu (50%) kwa wanawake ambao hawajawahi kuolewa. Vilevile, kuolewa katika umri mdogo kuna uhusiano wa moja kwa moja na viwango duni vya elimu ya msingi na ujuzi wa kusoma na kuandika


**Elimu, kwa umri ndoa ya kwanza, wanawake wenye miaka 15-49**




**Chanzo:** DHS 2015 -16


**Jambo la 6. Wananchi wengi wanaunga mkono wasichana kurudi shule baada ya kujifungua**

Wananchi saba kati ya kumi (71%) wanaunga mkono hoja ya wasichana wajawazito kuruhusiwa kuendelea na masomo yao: 62% wanaunga mkono



kuwa wasichana warudi shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua, 7% wanaunga mkono wasichana waendelee na masomo shuleni wakati wa ujauzito na 2% wangependa wahamishiwe shule.


**Nini kinapaswa kufanyika kwa msichana anayepata mimba akiwa shuleni?**




**Chanzo:** Utafiti unaofanyika kwa njia ya Simu za Mkononi wa *Sauti za Wananchi,* awamu ya 10 (Agosti 2016); Twaweza

**Jambo la 7. Ndoa za utotoni ndio sababu kuu ya kupata watoto katika umri mdogo**


Makadirio ya Benki ya Dunia yanadokeza kwamba watoto wawili kati ya watatu (65%) waliozaliwa na mama mwenye umri chini ya miaka 18 walitokana na ndoa za utotoni, na kwamba idadi sawa na hiyo (65%) ya wanawake waliopata watoto kabla ya umri wa miaka 18 ilikuwa ni matokeo ya ndoa za utotoni.




**Chanzo:** World Bank Tanzania Economic Update Jan 2019.


**Jambo la 8. Wanawake ambao wameolewa utotoni wana watoto wengi zaidi katika umri mdogo kuliko wanawake walioolewa wakiwa na umri mkubwa**

Kwa wastani, wanawake ambao waliolewa utotoni wana watoto watatu, na walipata mtoto wa kwanza wakiwa na umri wa miaka 17, wakati wanawake



waliolewa katika umri mkubwa wana watoto watatu, walianza kupata mtoto wa kwanza katika umri wa miaka 22. 58% ya wanawake waliolewa utotoni walipata watoto kabla ya kutimiza umri wa miaka 18 ikilinganishwa na 10% ya wanawake walioolewa wakiwa na umri wa miaka 20 au zaidi.

**Ndoa za mapema na upataji watoto mapema**






**Chanzo:** DHS 2015-16, takwimu zimechambuliwa na mwandishi


**Jambo la 9. Wasichana ambao huendelea na masomo shuleni kwa muda mrefu wana familia zenye afya bora**

Kiwango cha elimu cha mama kinahusishwa moja kwa moja na viashiria vingi vya kiafya ya familia zao. Akina mama waliopata elimu bora wana uwezekano mkubwa wa kujifungulia watoto wao kwenye kituo cha afya, kutafuta matibabu ya watoto, na watoto wao wana uwezekano mdogo wa kupata magonjwa ikiwemo ugonjwa wa malaria.

**Afya ya watoto, kwa kiwango cha elimu ya mama**









**Chanzo:** DHS 2015-16


Uchambuzi wa Benki ya Dunia unaonesha uwepo wa athari kubwa kutokana na ndoa za utotoni, kwa wasichana wenyewe na kwa watoto wao, na taifa kwa ujumla

Benki ya Dunia iligundua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ndoa za utotoni na elimu ya wasichana. Kupunguza ndoa za utotoni kunawawezesha wasichana kuendelea na masomo yao shuleni kwa muda mrefu, na kuendelea na masomo yao shuleni kwa muda mrefu kunasaidia kupunguza ndoa za utotoni.




**Chanzo:** World Bank Tanzania Economic Update Jan 2019

Aidha, kupunguza ndoa za utotoni na kuelimisha wasichana kunaweza kuleta matokeo chanya na makubwa kwa maisha yao ya baadaye, na maisha ya watoto na kaya zao kwa ujumla. Wasichana ambao huolewa katika umri mkubwa wanakuwa na elimu bora, wanapata kazi nzuri, wanakuwa na watoto wachache, watoto wao wanakuwa na afya bora, na wana ushawishi mkubwa



katika maamuzi muhimu kwenye ngazi ya kaya. Ushahidi zaidi wa kuunga mkono hoja hizi upo katika kitini hiki cha mambo muhimu.

Pamoja na hayo, wasichana wanapoolewa katika umri mkubwa, inaleta manufaa makubwa kwa taifa kwa ujumla. Watu watakuwa na afya njema na ustawi kwa ujumla ikiwa ndoa za utotoni zitakomeshwa, na itachangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza mzigo kwenye bajeti ya kitaifa.

Baadhi ya manufaa hayo yameelezwa hapa chini kwa ufupi:

↑ **6%**

"Kila mwaka ndoa za utotoni zinaongeza hatari ya wasichana kutomaliza elmu ya sekondari kwa asilimia pointi 6"

↓ **17%**

"Kila mwaka wa elimu ya sekondari unapunguza hatari ya kuolewa utotoni wasichana kwa asilimia pointi 17"

↓ **9%**

"Kila mwaka wa elimu ya sekondari unapunguza hatari ya msichana kuzaa mtoto akiwa bado mdogo kwa asilimia pointi 9"

Kwa kuzingatia uhusiano wa karibu kati ya kusoma zaidi, ndoa za utotoni, na kuzaa watoto mapema, hatua madhubuti za kupunguza kasi ya kuongezeka kwa ndoa ya utotoni na kuzaa watoto mapema inaonekana kuwa ni motisha kwa wasichana kuwa shuleni au kurudi shuleni.

↑ **22%**

"Kuhitimu elimu ya sekondari kwa wanawake wote kunawaongezea uwezo wa kufanya maamuzi kwa kwa 22%."

↓ **9%**

"Duniani, ndoa za utotoni hupunguza kipato cha mwanamke katika maisha yake kwa asilimia 9, hasa kwa sababu wanaoolewa mapema huacha shule mapema."

↑ **.9%**

"Kukomesha ndoa za utotoni kunaweza kuongeza mapato na tija kitaifa kwa asilimia 0.9."


**$637m**

"Nchini Tanzania, jumla ya thamani ya mapato yaliyopotea kutokana na ndoa za utotoni mwaka 2015 yalikuwa dola za Kimarekani milioni 637."

**$5bn**

"Faida za kiuchumi za kukomesha ndoa za utotoni (nchini Tanzania) ni kubwa sana katika nyanja za ustawi wa watu, wakiwa wanaongezeko kwa idadi ndogo: ifikapo mwaka 2030 inaweza kufikia dola bilioni 5 za Kimarekani kwenye faharasa ya uwezo wa kununua"


**Vyanzo:** World Bank Tanzania Economic Update Jan 2019 and Economic Impacts of Child Marriage: Global Synthesis Report, ICRW na Benki ya Dunia (2017)



**Jambo la 10. Wanawake walioolewa utotoni wana uwezekano mdogo wa kupata kazi ya kitaalam au inayohitaji ujuzi, wana uwezekano mkubwa wa kufanya kazi za kilimo**

Kwa wanawake ambao wameolewa utotoni, wanawake sita kati ya kumi (60%) hufanya kazi za kilimo, ikilinganishwa na wanawake wanne kati ya kumi (39%) ambao wameolewa wakiwa na umri wa miaka ishirini au zaidi. Tofauti na hiyo, wanawake walioolewa katika umri mkubwa (14%) wana uwezekano mkubwa wa kufanya kazi za kitaalam, kitaaluma au kazi zinazohitaji ujuzi kuliko wenzao walioolewa utotoni (3%).

**Kazi kuu za wanawake**





**Chanzo:** DHS 2015-16, takwimu zimechambuliwa na mwandishi


**Jambo la 11. Wanawake ambao wameolewa utotoni wana uwezo mdogo wa kufanya maamuzi muhimu katika familia zao**

Wanawake ambao wameolewa utotoni wana uhuru mdogo wa kuamua jinsi ya kutumia mapato yao kuliko wale ambao wameolewa katika umri mkubwa.

Vivyo hivyo, wanawake ambao wameolewa utotoni wana uwezekano mdogo wa kuwa na sauti juu ya namna ya kutumia mapato ya waume au wenza wao. Aidha, wanawake ambao wameolewa utotoni pia wana uwezekano mdogo wa kuwa na sauti katika maamuzi yanayohusiana na afya zao.



**Nyumbani kwako, nani anayeamua siku zote yafuatayo?**





**Chanzo:** DHS 2015-16, takwimu zimechambuliwa na mwandishi

**Jambo la 12. Wanawake ambao wameolewa utotoni wana uwezekano mkubwa wa kukubali kwamba ukatili dhidi ya wanawake majumbani unakubalika**


Kwa wanawake ambao wameolewa wakiwa watoto, nusu yao (47%) wanakubaliana kuwa ni sawa kwa mume kumpiga mkewe endapo atatoka kwenda mahali fulani bila kutoa taarifa, ikilinganishwa na 37% ya wanawake ambao wameolewa wakiwa na umri mkubwa.

Elimu ina nguvu zaidi katika hoja hii. Wanawake wenye elimu kubwa wana uwezekano mdogo wa kukubali kuwa ukatili majumbani unakubalika.

**Asilimia ya wanawake wanaosema ni sawa wanaume kuwapiga wake zao...**





**Chanzo:** DHS 2015-16, takwimu zimechambuliwa na mwandishi



**Jambo la 13. Wanawake walioolewa utotoni wana uwezekano mkubwa wa kusema ukatili wa majumbani unakubalika**

Vile vile, wanawake ambao wameolewa utotoni wana uwezekano mkubwa wa kufanyiwa ukatili na waume au wenza wao, pamoja na ukatili mkubwa wa kingono. Katika jambo hili, suala la elimu pia linaweza kuonekana, ingawa halina nguvu zaidi kuliko suala la umri wa kuolewa.

**Asilimia ya wanawake waliowahi kutendewa ukatili na waume/wenza wao.**





**Chanzo:** DHS 2015-16, takwimu zimechambuliwa na mwandishi

**Jambo la 14. Watu wanaotajwa zaidi kutenda ukatili wa kingono kwa wanawake ni wenza wao wa sasa na wa zamani**


Kati ya wanawake ambao wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono, wanawake wanne kati ya kumi (42%) wameripoti kuwa walifanyiwa ukatili huo zaidi na waume au wenza wao wa sasa, kuliko mtu mwingine yeyote.

Wanawake wengine watatu kati ya kumi (34%) wametaja mume au mwenza wa zamani, na mmoja kati ya kumi (11%) wanasema ni mpenzi wa sasa au wa zamani ndio wanaofanya ukatili wa kingono.

**Wahusika waliotajwa kutekeleza ukatili wa kingono kwa wanawake**




**Chanzo:** DHS 2015-16



## Jambo la 15. Mahakama Kuu ya Tanzania imetangaza kwamba sheria zinazoruhusu ndoa za utotoni siyo za kikatiba




Sheria ya Ndoa inasema kuwa msichana anaruhusiwa kuolewa akiwa na miaka 15 (wazazi wakikubali) na miaka 18 kwa wavulana.

Januari 2016, Rebeca Gyumi alileta kesi mahakamani, akidai kuwa sheria hii inakiuka katiba, kwa vile inaweka umri tofauti kwa ndoa kwa wasichana na wavulana.

Serikali ilijaribu kutetea sheria ilivyo kwa kusema inazingatia maadili ya kimila, kidini na kijamii. Mahakama ilikataa.


Baada ya kuangalia sheria mbalimbali zinazotamka umri wa mtoto, mahakama ilitoa uamuzi kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18.

Hivyo, mahakama iliamua kuwa kifungu namba 13 na 17 ya Sheria ya Ndoa vinakiuka katiba ya nchi.



IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM MAIN REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM
MISCELLANEOUS CIVIL CAUSE NO 5 OF 2016
IN THE MATTER OF THE CONSTITUTION OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA 1977 – AS AMENDED FROM TIME TO TIME (CAP. 2 R.E. 2002)
AND
IN THE MATTER OF BASIC RIGHTS AND DUTIES ENFORCEMENT ACT [CAP 3 R.E. 2002]
AND
IN THE MATTER OF A PETITION TO CHALLENGE CONSTITUTIONALITY OF SECTION 13 AND 17 OF THE LAW OF MARRIAGE ACT (CAP 29 R.E. 2002)
BETWEEN
REBECA Z. GYUMI .................... APPLICANT
VERSUS
THE ATTORNEY GENERAL .................... RESPONDENT
JUDGMENT
Date of Last Order: 3/3/2016

Baada ya kuona kwamba msichana chini ya miaka 18 ni mtoto, tumekubali kuwa haipaswi kumfanya awe na majukumu mazito ya kindoa



**Jambo la 16. Tanzania imesaini mikataba kadhaa ya kimataifa ambayo inaitaka nchi ichukue hatua kumaliza tatizo la ndoa za utotoni**

**Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948)**

Wanawake na wanaume wanastahili haki sawa za ndoa, wakati wanapokuwa kwenye ndoa na hata ndoa inapovunjika. Mtu ataingia katika ndoa kwa ridhaa yake kamili na ridhaa ya mwenza wake mtarajiwa bila kulazimishwa.

**Azimio la Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW; 1979)**

Azimio hili linazitaka serikali zichukue hatua madhubuti kuhakikisha kwamba “kuposwa na kuolewa kwa mtoto hakutakubalika kisheria

**Azimio la Haki za Mtoto (1989)**

Azimio hili linamuelezea mtoto kama ni mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18, na linasema kuwa katika mambo yote yanayohusiana na watoto, maslahi bora ya mtoto yatakua ya msingi na yatapewa kipaumbele. Pia linabainisha kuwa watoto wanayo haki ya kupata elimu kwa usawa na haki sawa, kulindwa dhidi ya unyanyasaji wowote wa kijinsia na ukatili wa kingono, na kulindwa dhidi ya kila aina ya ukatili wa hali yoyote ya ustawi wa mtoto.

**Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu UN (SDGs; 2015)**

Lengo la 5.3 linazielekeza nchi zote wanachama kumaliza kabisa tatizo la ndoa za utotoni ifikapo mwaka 2030.

**Mkataba wa Afrika kuhusu Itifaki ya Haki za Binadamu na Haki za Wanawake (2003)**

Makubaliano haya yanasema kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kuwa washirika wenye haki sawa katika ndoa, na lazima pande zote mbili zitoe ridhaa ya maandishi. Ridhaa hiyo inaweza kutolewa na watu wazima tu, wenye umri wa miaka zaidi ya 18.